



# KUKAA NYUMBANI UKIWA NA COVID-19 CHANJO NA BUSTA

Je, wewe au mtu unayemjua anamtunza mtu aliye na ugumu wa kutoka nyumbani? Ratibu chanjo ya BILA MALIPO ya COVID-19 ukiwa nyumbani!

## Ni nani anastahili kupata chanjo akiwa nyumbani?

### Kila mtu aliye na umri wa miezi 6 na zaidi ambaye:

- Anastahiki kupokea misururu ya msingi au dozi ya busta **na**
- Ana maradhi makali au ya kudumu, hawesi kutembea, ana jeraha, ana ulemavu wa kukua, au hali ya afya ya kiakili ambayo hufanya awe na ugumu wa kutoka nyumbani.

**Dozi zote za msingi na za busta zinapatikana BILA MALIPO kwa chanjo ya nyumbani licha ya bima, uraia, au hali ya uhamiaji.**

## Nawezaje kuomba miadi ya chanjo ya nyumbani?

- Piga simu kwa **206-848-0243**, siku za wiki, kuanzia saa 2:30 asubuhi hadi saa 11:30 jioni (sema lugha unayopendelea ukiunganishwa).
- Iwapo una ulemavu na unahitaji malazi, tuma barua pepe kwa **publichealthaccommodations@kingcounty.gov** au piga simu kwa nambari **206-848-0243** (tuambie unachohitaji ukiunganishwa).

Updated: 05/17/2023